TANGAZO LA SERIKALI NA. 365 la tarehe 10/05/2024

SHERIA YA CHUO CHA ELIMU YA BIASHARA
(SURA YA 315)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 14(1))*

KANUNI ZA NIDHAMU KWA WANAFUNZI ZA MWAKA 2024

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

## SEHEMU YA PILI

## MAKOSA YA KINIDHAMU

4. Makosa ya kinidhamu.
5. Makosa yanayohusiana na utaratibu wa mavazi.
6. Makosa yanayohusiana na malazi.
7. Kumfukuza mwanafunzi bwenini.
8. Uharibifu au upotevu wa mali ya Chuo.
9. Haki ya kuvunja mkataba wa upangaji

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YANAYOHUSIANA NA MGAHAWA NA JIKO

10. Zuio la kuingia jikoni.

SEHEMU YA NNE
MASUALA YA KITAALUMA NA MAWASILIANO

11. Kuripoti chuoni.
12. Kutokuwepo chuoni.
13. Mawasiliano rasmi.
14. Taarifa ya vikao.
15. Huduma za Maktaba.

SEHEMU YA TANO
KAMATI YA NIDHAMU NA MAMLAKA YAKE

16. Kuanzishwa kwa Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi.
17. Ushirikishwaji wa mtu mwingine.
18. Majukumu ya Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi.
19. Vikao vya Kamati.
20. Uamuzi wa Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi.

SEHEMU YA SITA
TARATIBU ZA MASHAURI YA KINIDHAMU

21. Taarifa kutolewa kwa maandishi.
22. Uchunguzi wa awali.
23. Hati ya mashtaka kusomwa.
24. Ushahidi.
25. Kuwaita mashahidi.
26. Kukiri kosa.
27. Uamuzi wa Kamati.

SEHEMU YA SABA
RUFAA

28. Kuanzishwa kwa Kamati ya Rufaa ya Nidhamu kwa Wanafunzi.
29. Majukumu ya Kamati ya rufaa.
30. Rufaa.
31. Uamuzi wa Rufaa.

32. Uamuzi wa Kamati ya Rufaa ya Nidhamu kwa Wanafunzi.

SEHEMU YA NANE
ADHABU

33. Adhabu.
34. Makosa ya jinai.

SEHEMU YA TISA
MASHARTI MENGINEYO

35. Matumizi ya sheria nyingine za Chuo.
36. Mwanafunzi kurejea Chuo baada ya kusimamishwa.
37. Usalama maeneo ya Chuo.

SHERIA YA CHUO CHA ELIMU YA BIASHARA,
(SURA YA 315)

KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 14(1))*

KANUNI ZA NIDHAMU KWA WANAFUNZI ZA MWAKA 2024

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Nidhamu kwa Wanafunzi za Mwaka 2024.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika kwa wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"afisa aliyeidhinishwa" maana yake ni afisa yeyote wa Chuo aliyeidhinishwa kutekeleza majukumu ya Chuo;

"afisa Ustawi wa Jamii" maana yake ni afisa anayefanya kazi katika ofisi ya Mshauri wa Wanafunzi au Kurugenzi ya Huduma za Wanafunzi;

"Baraza la Wanafunzi" maana yake ni mkutano mkuu wa wanafunzi unaowahusisha wanafunzi wote wa Chuo au wanafunzi katika kampasi husika;

"Bodi ya Uongozi" maana yake ni Bodi ya Uongozi wa Chuo cha Elimu ya Biashara;

"kosa la kinidhamu" maana yake ni kosa lililokatazwa chini ya Kanuni hizi;

"mabweni" maana yake ni majengo ya Chuo au makazi yaliyokodiwa kwa ajili ya malazi ya wanafunzi;

"Mkurugenzi wa kampasi" maana yake ni mkuu wa usimamizi wa kampasi husika isipokuwa kampasi

kuu;

"Mshauri wa Wanafunzi" maana yake ni afisa anayesimamia masuala na huduma za wanafunzi na inajumuisha Mkurugenzi wa Huduma za Wanafunzi;

"mwanafunzi" maana yake ni mtu aliyesajiliwa kikamilifu na Chuo kufanya programu yoyote ya kitaaluma;

Sura ya 315

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Chuo cha Elimu ya Biashara; na

"silaha" maana yake silaha ya moto, kisu, panga, rungu, kipande cha chuma na nyingine za aina hiyo.

## SEHEMU YA PILI
## MAKOSA YA KINIDHAMU

Makosa ya kinidhamu

4. Kwa madhumuni ya Kanuni hizi, makosa ya kinidhamu yatajumuisha-

(a) mwenendo ambao unafanya au una uwezekano wa kusababisha uharibifu au vurugu kwa mtu au mali yoyote ndani ya Chuo ikizingatiwa kuwa, kitendo hicho kimefanywa na mwanafunzi dhidi ya mwanafunzi mwingine au afisa, chuoni au eneo lolote lililokodishwa au linalotambuliwa rasmi na Chuo;

(b) kutumia nguvu, vurugu au vitisho dhidi ya au kumshambulia mwanafunzi mwingine au afisa wa Chuo au mtu yeyote ndani ya Chuo au eneo lolote lililokodishwa au linalotambuliwa rasmi na Chuo;

(c) kitendo au mwenendo ambao unaweza kuzuia au kukwamisha kufanyika kwa shughuli yoyote ya kitaaluma, kiutawala au uchaguzi;

(d) kuharibu, kufuja au kuvuruga mali ya Chuo;

(e) matumizi yasioidhinishwa ya, au kuingilia, mfumo wowote wa kiteknolojia, umeme au huduma zingine za Chuo;

(f) kumiliki mali yoyote ya Chuo bila kibali;

(g) kukataa au kushindwa kutii amri halali au maelekezo yaliyotolewa na afisa yeyote wa Chuo au amri kutoka kwa chombo chochote husika cha Chuo;

(h) kwa makusudi na kwa kujua, kutoa taarifa ya uongo;

(i) kushindwa au kukataa kuhudhuria kikao kilichoitishwa na chombo chochote chenye mamlaka kwa njia ya mdomo au maandishi;

(j) kuzuia au kuingilia kwa makusudi kazi au mashauri yaliyoendeshwa na afisa yeyote mwenye mamlaka au chombo chochote chenye mamlaka cha Chuo;

(k) kukataa au kushindwa kutoa ushahidi mbele ya Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi au chombo chochote chenye mamlaka;

(l) kukataa au kushindwa kuheshimu na kutekeleza hukumu, uamuzi au adhabu halali iliyotolewa na afisa yeyote au chombo chochote chenye mamlaka;

(m) mwanafunzi kutumia lugha ya kashfa, matusi au ya kitisho dhidi ya mwanafunzi mwingine, afisa au mwanajumuiya yeyote wa Chuo;

(n) kutenda kwa namna ambayo inaweza kushawishi au kuchochea vurugu miongoni mwa wanafunzi, iwe ndani ya Chuo au eneo lolote lililokodishwa au linalotambuliwa rasmi na Chuo;

(o) kufanya kitendo chochote ambacho kinasababisha au kinaweza kusababisha madhara ya kimwili au kisaikolojia kwa mwanafunzi mwingine, afisa wa chuo au mwanajumuiya yeyote wa Chuo;

(p) kupiga kelele, kusumbua au kuwahamasisha wanafunzi au watu wengine kupiga kelele au kufanya usumbufu wa aina yoyote kwenye majengo ya Chuo au majengo

yoyote yaliyokodiwa;

(q) kuunda au kuanzisha kikundi cha wanafunzi kisichoruhusiwa ambacho kinaweza kusababisha kuvunja umoja au kuleta vurugu;

(r) kuandaa, kushiriki au kuitisha kwa makusudi mkutano au kikao kinyume na sheria;

(s) kuchochea na kushiriki katika ghasia, mgomo, kususia madarasa, au kushiriki kwenye vurugu au uchochezi wowote;

(t) kushawishi wanafunzi kugomea suala lolote;

(u) kuitisha au kufanya Baraza la Wanafunzi bila ruhusa;

(v) kupanga au kushiriki kwenye maandamano yasiyo halali;

(w) kumwalika kiongozi wa serikali au wa kisiasa, mgeni rasmi, mshereheshaji, au mtu yeyote kutoka nje ya Chuo bila kupata ruhusa kutoka kwa Mshauri wa Wanafunzi au afisa mwingine yeyote mwenye mamlaka;

(x) kusambaza kwa maandishi au mdomo matamko ya kashfa kwa watu wengine;

(y) uzembe au ubadhirifu wa fedha za Serikali ya Wanafunzi au chama, klabu, au kikundi chochote cha wanafunzi kinachotambulika;

(z) kiongozi wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara kuingia mkataba na mtu yeyote kinyume na Katiba ya Serikali ya Wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara;

(aa) kukusanya fedha kwa ulaghai au kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kutoka kwa wanafunzi wenzake au mtu mwingine yeyote;

(bb) kushindwa kulipa fidia kwa uharibifu au upotevu wa mali ya Chuo;

(cc) kubeba silaha bila ruhusa au kibali ndani ya majengo ya Chuo au eneo lolote lililokodishwa au linalotambuliwa rasmi na Chuo;

(dd) wizi unaofanyika katika majengo ya Chuo au eneo lolote lililokodishwa au linalotambuliwa rasmi na Chuo;

(ee) kughushi waraka, kusambaza waraka wa uongo au kuwasilisha waraka wa kughushi;

Sura ya 273

(ff) kosa ambalo linavunja Sheria ya Serikali Mtandao;

(gg) kutumia dawa zozote haramu au sumu ya aina yoyote kwa mwanafunzi mwenyewe au mwanafunzi mwenzake au mtu mwingine yeyote;

Sura ya 443

(hh) kosa ambalo linavunja Sheria ya Makosa ya Kimtandao;

(ii) kitendo chochote kinachofanywa na mwanafunzi ndani au nje ya Chuo na kupelekea kuharibu taswari ya Chuo;

(jj) kuendesha mkutano au kampeni ya uchaguzi nje ya muda uliopangwa;

(kk) unyanyasaji wa kijinsia wa aina yoyote ikijumuisha -

(i) kushinikiza kufanya tendo la ngono au upendeleo;

(ii) kuuliza kuhusu maisha binafsi ya kingono, kushawishi kupewa ngono kwa ahadi ya kutoa zawadi;

(iii) kutoa maoni ya udhalilishaji kutokana na umbo la mtu, kung'ang'ania kuomba miadi;

(iv) kufanya utani wa kingono, kutoa maoni ya kingono, kutumia lugha ya matusi, kutoa ishara ya kingono;

(v) kusema uongo au kueneza uvumi kuhusu maisha ya kingono ya mtu kwa madhumuni ya kuharibu sifa za mlengwa;

(vi) kugusana kimwili kwa kusudio la kingono bila ridhaa;

(vii) kusambaza ujumbe wa shambulizi ya kingono kwa njia yoyote;

(viii) kufanya ngono ya kundi;

(ix) kubaka au shambulio la aibu au kuwa uchi au kubaka kwa kundi;

(x) matumizi ya mamlaka au madaraka kumshawishi mtu mwingine kuingia katika mahusiano ya kingono au kumuadhibu mtu kutokana na kukataa kwake.

(ll) kuomba au kutoa rushwa ya ngono;

(mm) kujifanya mtu mwingine;

(nn) kitendo chochote cha mwanafunzi chenye lengo la kuonesha ushiriki au utii kwa chama cha siasa;

(oo) kushawishi au kuwachochea wanafunzi kugomea mihadhara, mitihani ya vitendo au kazi yoyote ya kitaaluma;

(pp) kushindwa kusoma taarifa au matangazo kwenye ubao wa matangazo, mfumo wa habari wa wanafunzi, tovuti ya Chuo au namna nyingine itakayotumika, au kushindwa kufuata maelekezo ya Chuo;

Sura ya 95

(qq) kosa ambalo linavunja Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya;

Sura ya 329

(rr) kosa ambalo linavunja Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa;

(ss) kuingilia pasipo uhalali mchakato wa uchaguzi wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara.);

(tt) kuunda au kuanzisha chama, klabu au kikundi cha wanafunzi bila ruhusa kutoka kwa Mshauri wa Wanafunzi, afisa ustawi wa jamii au chombo chochote chenye mamlaka;

(uu) kushindwa kuonesha au kukabidhi kitambulisho cha uanafunzi inapotakiwa

kufanya hivyo na afisa mwenye mamlaka;

(vv) kutokupitisha kwa Mshauri wa Wanafunzi au afisa ustawi wa jamii mawasiliano yoyote rasmi ya kwenda nje ya Chuo kwa mwanafunzi yeyote au kiongozi wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo cha Biashara; na

(ww) kushindwa kurejesha mkopo au deni baina ya wanafunzi au mtu mwingine yeyote.

Makosa yanayohusiana na utaratibu wa mavazi

5. Wanafunzi hawaruhusiwa kuvaa mavazi yafuatayo katika maeneo ya Chuo au eneo lolote lililokodishwa au linalotambuliwa rasmi na Chuo:

(a) jinzi au nguo yenye matundu;
(b) nguo yenye matundu au inayoonesha ndani;
(c) suruali za kuning'inia chini ya makalio;
(d) suruali, sketi au blauzi za kubana;
(e) gauni au sketi yenye mpasuo mrefu kupita kiasi;
(f) nguo inayoacha tumbo, kiuno, matiti, kifua na mgongo wazi;
(g) kaptura au sketi ambayo haifuniki mapaja akiwa amekaa;
(h) aina yoyote ya vipedo au pedo-pusha;
(i) nguo inayobana mwili;
(j) nguo inayofunika uso;
(k) hereni za masikio au za pua kwa mwanafunzi wa kiume;
(l) nguo inayoonyesha nguo ya ndani;
(m) pajama au nguo za kulalia zinapovaliwa nje ya bweni;
(n) kofia kuvaliwa darasani, ofisini, maktaba, kwenye kikao, maabara au kwenye mkutano wowote rasmi;
(o) nguo yenye picha au kaulimbiu isiyostahili au lugha isiyo na staha au ya matusi;
(p) mtindo wa nywele usiofaa kwa wanaume; na
(q) aina yoyote ya uvaaji ambao afisa wa Chuo ataona haufai.

Makosa yanayohusiana na malazi

6. Makosa ya kinidhamu yanayohusiana na malazi yatajumuisha-

(a) kupangisha chumba katika mabweni ya Chuo au malazi mengine yaliyokodiwa au kutambuliwa na Chuo kwa mtu mwingine;

(b) kuishi kwenye bweni la Chuo au malazi mengine yaliyokodiwa au kutambuliwa na Chuo pasipo uhalali;

(c) kutumia majengo ya mabweni kwa ajili ya matukio ya kijamii bila kupata kibali cha Mshauri wa Wanafunzi au afisa Ustawi wa Jamii;

(d) kuchangia chumba na mwanafunzi wa jinsia tofauti;

(e) kupika chakula bwenini pasipo kibali cha maandishi kutoka kwa Mshauri wa Wanafunzi au afisa Ustawi wa Jamii;

(f) kuingilia au kuhamisha samani au vifaa vya aina yoyote kutoka bwenini bila ruhusa ya Mshauri wa Wanafunzi au afisa Ustawi wa Jamii;

(g) kutumia baraza, dirisha au ukuta kwa ajili ya kuanika nguo au ufuaji wa aina yoyote;

(h) kuingiza bwenini friji, mashine ya kukausha nywele, jokofu au kifaa chochote cha kupikia pasipo kibali cha maandishi kutoka kwa Mshauri wa Wanafunzi au afisa Ustawi wa Jamii;

(i) kuondoka bila kukabidhi vifaa vya malazi kwa afisa mwenye mamlaka;

(j) kumzuia afisa wa Chuo au mtu yeyote aliyeidhinishwa kuingia chumbani kwa ajili ya ukarabati, ukaguzi au shughuli nyingine kama ilivyoamuriwa;

(k) kutumia vifaa vya muziki na vyombo vingine vinavyotoa sauti bwenini na kusababisha usumbufu kwa wakazi wengine;

(l) ulevi, au uvutaji wa sigara bwenini; na

(m) kuwakaribisha wageni wa jinsia tofauti bwenini baada ya saa nne usiku.

Kumfukuza mwanafunzi bwenini

7. Mshauri wa Wanafunzi atakuwa na mamlaka ya kumfukuza mwanafunzi kwenye chumba cha bweni kwa muda wakati akisubiri uamuzi wa Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi au rufaa kama ipo.

Uharibifu au upotevu wa mali ya Chuo

8. Endapo uharibifu au upotevu wa mali ya Chuo umesababishwa na mwanafunzi ambaye utambulisho wake haujulikani, gharama za kukarabati au kubadili mali hiyo zitachangiwa na wanafunzi wote waliokuwepo wakati wa uharibifu au upotevu huo ukitokea.

Haki ya kuvunja mkataba wa upangaji

9. Chuo kitakuwa na haki ya kuvunja mkataba wa upangaji bila kutoa notisi na ada ya bweni haitarejeshwa pale mwanafunzi atakapohama, atakapoahirisha masomo, atakaposimamishwa, au kufukuzwa masomo.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YANAYOHUSIANA NA MGAHAWA NA JIKO

Zuio la kuingia jikoni

10.-(1) Mwanafunzi haruhusiwi kuingia jikoni kwa mtoa huduma za mgahawa bila ruhusa ya mtoa huduma au Mshauri wa Wanafunzi au Afisa Ustawi wa Jamii.

(2) Huduma ya mgahawa itakuwa katika maeneo yaliyopangwa kwa ajili ya huduma hiyo na mwanafunzi haruhusiwi kuchukua chombo au kitu chochote kutoka mgahawani au eneo lolote ndani au nje ya Chuo bila ruhusa ya mtoa huduma.

(3) Ukosoaji au malalamiko au maoni kuhusu huduma za mgahawa yatapelekwa kwa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara kwa maandishi na nakala yake kuwasilishwa kwa Mshauri wa Wanafunzi.

(4) Baada ya kupokea maoni au malalamiko kwa mujibu wa masharti ya kanuni ndogo ya (3), Mshauri wa Wanafunzi atachukua hatua stahiki.

## SEHEMU YA NNE
## MASUALA YA KITAALUMA NA MAWASILIANO

Kuripoti chuoni

11.-(1) Wanafunzi wote watatakiwa kuripoti chuoni mwanzoni mwa kila muhula kwa tarehe iliyopangwa na Chuo.

(2) Mwanafunzi ambaye amepata udahili wa Chuo na amesajiliwa kwenye programu maalumu hataruhusiwa kubadili programu ambayo amesajiliwa bila idhini ya maandishi ya Chuo kwa kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Kutokuwepo chuoni

12.-(1) Ruhusa ya kutokuwepo chuoni kwa sababu yoyote inayohusisha kukosa vipindi vya masomo au kazi yoyote ya kitaaluma itaombwa kwa maandishi kwa Mkurugenzi wa Taaluma au Mkurugenzi wa Kampasi kupitia kwa Mkuu wa Idara ya Taaluma husika na kupeleka nakala kwa Mshauri wa Wanafunzi au afisa Ustawi wa Jamii.

TS Na. 927 la 2023

(2) Masharti ya kanuni ndogo ya (1), hayataathiri matakwa ya Kanuni za Mitihani za Chuo.

Mawasiliano rasmi

13. Mawasiliano yoyote rasmi kwenda nje ya Chuo yanayofanywa na mwanafunzi au Serikali ya Wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara kuhusu suala lolote linalohusu maslahi ya wanafunzi au Chuo kwa ujumla yatapitia kwa Mshauri wa Wanafunzi au afisa Ustawi wa Jamii.

Taarifa ya vikao

14. Vikao, mkutano, semina au kusanyiko lolote baina ya mwanafunzi na mamlaka ya nje ya Chuo ambapo masuala ya Chuo yatajadiliwa ni lazima litanguliwe na taarifa ya maandishi ya siku tatu kabla ya tukio husika kwenda kwa Mkuu wa Chuo au Mkurugenzi wa Kampasi ikionesha nia ya kufanya tukio hilo, ikitaja mamlaka ya nje, mambo yatakayojadiliwa, muda na mahali pa tukio hilo.

Huduma za

15.-(1) Huduma za Maktaba chuoni zitatolewa

Maktaba

kwa wanafunzi kwa saa maalumu za kazi kama Chuo kitakavyoainisha.

(2) Mwanafunzi atakayeazima kitabu, jarida, gazeti, nyaraka yoyote au kifaa cha Maktaba ya Chuo atawajibika binafsi kukitunza, kukilinda na kukirejesha bila kuharibiwa kwa tarehe iliyotajwa au iliyokubaliwa kurejesha.

## SEHEMU YA TANO
## KAMATI YA NIDHAMU NA MAMLAKA YAKE

Kuanzishwa kwa Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi

16.-(1) Kunaanzishwa Kamati itakayojulikama kama Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi.

(2) Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi itaundwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mkuu wa Usimamizi wa Rasilimali Watu kwenye Kampasi ambaye atakuwa Mwenyekiti;
(b) mtu mmoja aliyeteuliwa na Chama cha Wafanyakazi Wanataaluma kutoka miongoni mwa wanachama wake;
(c) wanafunzi wawili mmoja wa kike na mmoja wa kiume walioteuliwa na Serikali ya Wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara;
(d) Mkuu wa udahili au mwakilishi wake ambaye atakuwa Katibu;
(e) mwakilishi kutoka idara ambayo mwanafunzi anayeshtakiwa anatoka; na
(f) mwakilishi kutoka Kitengo cha Huduma za Kisheria chuoni au mfanyakazi yeyote mwenye taaluma ya sheria.

Ushirikishwaji wa mtu mwingine

17.-(1) Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi inaweza kumualika mtu yeyote kuhudhuria kikao chake endapo italazimu.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mtu aliyealikwa hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Majukumu ya Kamati ya

18. Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi itakuwa na majukumu yafuatayo:

Nidhamu kwa Wanafunzi

(a) kupokea na kujadili suala la kinidhamu la mwanafunzi yeyote kama litakavyowasilishwa na Mshauri wa Wanafunzi au mtu mwingine yeyote aliyeteuliwa kwa madhumuni hayo;

(b) kumwita na kumhoji mwanafunzi yeyote au mtu mwingine, na kudai ushahidi unaohusiana na tuhuma husika;

(c) kuanzisha mashauri ya kinidhamu kwa mwanafunzi yeyote chini ya Kanuni hizi;

(d) kutoa adhabu stahiki kwa mwanafunzi kwa kosa lililothibitika chini ya Kanuni hizi;

(e) kushauri Chuo na kutoa mapendekezo kuhusu masuala ya kinidhamu ya wanafunzi; na

(f) kufanya mambo mengine yoyote kwa ajili ya kudumisha na kuhimiza nidhamu miongoni mwa wanafunzi wa Chuo.

Vikao vya Kamati

19.-(1) Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi itakuwa na mamlaka ya kuitisha vikao wakati wowote itakapohitajika.

(2) Nusu ya wajumbe itaunda akidi katika kikao cha Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi.

(3) Uamuzi wa wajumbe walio wengi waliohudhuria na kupiga kura kwenye kikao utachukuliwa kuwa uamuzi wa Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi.

(4) Endapo itatokea kura kulingana, Mwenyekiti wa kikao atakuwa na kura ya turufu.

Uamuzi wa Kamati ya Nidhamu ya Wanafunzi

20. Mwenyekiti wa Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi atamjulisha Mkuu wa Chuo au Mkurugenzi wa Kampasi kuhusu uamuzi wa Kamati.

## SEHEMU YA SITA
## TARATIBU ZA MASHAURI YA KINIDHAMU

Taarifa kutolewa kwa maandishi

21.-(1) Kosa lolote la kuvunja Kanuni hizi litaripotiwa kwanza kwa maandishi kwa Mshauri wa Wanafunzi au afisa Ustawi wa Jamii ambaye

atashughulikia kosa hilo kiutawala au ikibidi, atapeleka shauri hilo mbele ya Kamati ya Nidhamu kwaa Wanafunzi.

(2) Endapo mwanafunzi hakuridhika na hatua za kiutawala zilizochukuliwa na Mshauri wa Wanafunzi au afisa Ustawi wa Jamii, atamwomba kwa maandishi Mshauri wa Wanafunzi au afisa Ustawi wa Jamii husika apeleke shauri hilo mbele ya Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi; na Mshauri wa Wanafunzi au afisa Ustawi wa Jamii atatakiwa kutekeleza.

Uchunguzi wa awali

22.-(1) Baada ya tuhuma za kinidhamu kuripotiwa, Mshauri wa Wanafunzi au afisa Ustawi wa Jamii atafanya uchunguzi wa awali wa tuhuma hiyo.

(2) Baada ya uchunguzi wa awali kufanyika na kuonekana kwamba kuna tuhuma za kujibu, Mshauri wa Wanafunzi au afisa Ustawi wa Jamii-

(a) ataandaa na kusaini notisi na hati ya mashtaka dhidi ya mwanafunzi anayetuhumiwa;
(b) ataandaa ushahidi wa tuhuma husika; na
(c) atampatia mwanafunzi anayetuhumiwa notisi na hati ya mashtaka inayohitaji utetezi kwa maandishi.

(3) Mwanafunzi anayetuhumiwa atawasilisha utetezi wake ndani ya siku tatu za kazi tangu kupokea notisi na hati ya mashtaka.

Hati ya Mashtaka kusomwa.

23.-(1) Wakati wa kuanza kwa shauri la kinidhamu, Katibu atasoma shtaka, na kumtaka mwanafunzi mtuhumiwa kujibu kosa analotuhumiwa kama ni kweli au sio kweli.

(2) Endapo Mwanafunzi amekiri kutenda kosa, atatakiwa kujaza Fomu ya kukiri kosa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza na ataadhibiwa ipasavyo.

(3) Endapo mwanafunzi mtuhumiwa hayupo, na alipewa na kupokea notisi na hati ya shitaka ipasavyo, Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi itaendelea kusikiliza shauri hilo bila mwanafunzi mtuhumiwa kuwepo na

kuendelea kuamua ipasavyo.

(4) Endapo shauri hilo litaamuliwa kulingana na masharti ya kanuni ndogo ya (3), mwanafunzi mtuhumiwa atachukuliwa kuwa ameacha kutumia haki yake ya kusikilizwa, na kutetea shauri lake mbele ya Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi.

Ushahidi

24.-(1) Mlalamikaji atatoa maelezo juu ya shauri husika na kutoa ushahidi au kuleta mashahidi pale itakapobidi.

(2) Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi itatoa fursa kwa mwanafunzi anayetuhumiwa kumuuliza maswali mlalamikaji na shahidi wake, ikiwa yupo.

(3) Mwanafunzi mtuhumiwa atakuwa na haki ya kujitetea, kutoa ushahidi, na kumleta shahidi, ikiwa yupo.

(4) Wakili au mwakilishi yeyote haruhusiwi kumwakilisha mtuhumiwa chini ya Kanuni hizi.

Kuwaita mashahidi

25.-(1) Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi inaweza kuita shahidi yeyote kutoa ushahidi ipasavyo.

(2) Ushahidi unaweza kuchukuliwa na Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi kwa mdomo, maandishi, au kielektroniki isipokuwa kwamba, endapo ushahidi wa mdomo utachukuliwa, utawekwa katika maandishi.

Kukiri kosa

26. Endapo mwanafunzi mtuhumiwa amekiri kosa, masharti ya kanuni ya 23 (2) yatafuatwa.

Uamuzi wa Kamati

27. Uamuzi wa Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi utatolewa ndani ya siku saba za kazi kutoka tarehe ya kuhitimishwa kwa shauri la kinidhamu.

## SEHEMU YA SABA
## RUFAA

Kuanzishwa kwa Kamati ya Rufaa ya Nidhamu kwa Wanafunzi

28.-(1) Kunaazishwa Kamati ya rufaa itakayojulikana kama Kamati ya Rufaa ya Nidhamu kwa Wanafunzi.

(2) Kamati ya Rufaa ya Nidhamu kwa Wanafunzi

itaundwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti wa Kamati ya Bodi ya Uongozi inayosimamia masuala ya wanafunzi au mjumbe yeyote wa Bodi ya Uongozi au Mkurugenzi wa Kampasi ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) Mkurugenzi wa Huduma za Msaada wa Kitaaluma ambaye atakuwa Katibu;

(c) mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Mkuu wa Chuo;

(d) mwanafunzi mmoja atakayeteuliwa na Serikali ya Wanafunzi wa Chuo cha Biashara;

(e) mjumbe mmoja atakayeteuliwa kutoka nje ya Chuo mwenye uzoefu katika masuala ya wanafunzi kutoka taasisi za elimu ya juu;

(f) mwakilishi kutoka kitengo cha Huduma za Sheria ndani ya Chuo ambaye hakuwa sehemu ya Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi kuhusu rufaa husika.

Majukumu ya Kamati ya rufaa

29.Kamati ya Rufaa ya Nidhamu kwa Wanafunzi itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kupokea na kujadili rufaa iliyowasilishwa kupinga uamuzi wa Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi;

(b) kutoa uamuzi stahiki kwa mujibu wa Kanuni hizi juu ya rufaa iliyowasilishwa;

(c) kushauri Chuo na kutoa mapendekezo kuhusu masuala ya kinidhamu ya wanafunzi; na

(d) kufanya masuala mengine yoyote kwa lengo la kudumisha na kuhimiza nidhamu miongoni mwa wanafunzi.

Rufaa

30.-(1) Upande wowote ambao haujaridhika na uamuzi wa Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi chini ya Kanuni hizi unaweza kukata rufaa kwa Kamati ya Rufaa ya Nidhamu kwa Wanafunzi kupitia kwa Mkuu wa Chuo au Mkurugenzi wa Kampasi ndani ya siku saba za kazi

kutoka tarehe ya kupokea uamuzi wa Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), rufaa haitaruhusiwa endapo mkata rufaa alikiri kutenda kosa na kutiwa hatiani kwa kukiri huko mbele ya Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi isipokuwa kama ni kuhusu kiwango au uhalali wa adhabu.

(3) Mkuu wa Chuo au Mkurugenzi wa Kampasi atakuwa na mamlaka ya kukataa kwa maandishi rufaa yoyote iliyowasilishwa nje ya siku saba za kazi tangu kupokea uamuzi wa Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi.

(4) Rufaa itakayowasilishwa mbele ya Kamati ya Rufaa ya Nidhamu kwa Wanafunzi itakuwa kwa maandishi na itaweka sababu ya rufaa hiyo.

(5) Rufaa yoyote chini ya Kanuni hizi inaweza isipokelewe endapo haijaambatishwa na wasilisho la maandishi kuunga mkono rufaa hiyo kwa kuzingatia mojawapo ya sababu zifuatazo:

(a) Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi haikuundwa ipasavyo;
(b) hakukuwa na ushahidi wa kutosha wa kumtia hatiani mkata rufaa;
(c) kulikuwa na uvunjaji wa kanuni ya haki ya msingi;
(d) kukiri kwa mkata rufaa kulikuwa na utata; na
(e) kiwango au uhalali wa adhabu.

(6) Kamati ya Rufaa ya Nidhamu kwa Wanafunzi itakutana ndani ya saa ishirini na nane za kazi kutoka tarehe ya kupokea rufaa.

(7) Kamati ya Rufaa ya Nidhamu kwa Wanafunzi inaweza kumualika mtu yeyote kuhudhuria kikao chake endapo italazimika, isipokuwa kwamba katika kufanya maamuzi mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

(8) Akidi ya kikao cha Kamati ya Rufaa ya Nidhamu kwa Wanafunzi itakuwa nusu ya wajumbe wake halali.

Uamuzi wa rufaa

31.-(1) Adhabu yoyote iliyotolewa na Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi itaendelea kuwa halali mpaka

pale rufaa, ikiwa ipo, itaamuliwa vinginevyo.

(2) Kamati ya Rufaa ya Nidhamu kwa Wanafunzi itatoa uamuzi wa rufaa kwa kuzingatia kumbukumbu za Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi.

(3) Wakati wa kusikilizwa kwa rufaa haitakuwa lazima kwa mkata rufaa kuhudhuria.

Uamuzi wa Kamati ya Rufaa ya Nidhamu kwa Wanafunzi

32.-(1) Katika kuamua rufaa iliyowasilishwa chini ya Kanuni hizi, Kamati ya Rufaa ya Nidhamu kwa Wanafunzi itakuwa na mamlaka ya kuthibitisha, kubadili, au kubatilisha uamuzi wa Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi.

(2) Uamuzi wa Kamati ya Rufaa ya Nidhamu kwa Wanafunzi utatolewa ndani ya siku kumi za kazi kutoka tarehe ya kuhitimishwa kwa shauri la rufaa.

(3) Uamuzi wa Kamati ya Rufaa ya Nidhamu kwa Wanafunzi utakuwa ndiyo uamuzi wa mwisho.

## SEHEMU YA NANE
## ADHABU

Adhabu

33.-(1) Baada ya kuthibitika kwa kosa lolote chini ya Kanuni hizi, Mamlaka husika itatoa adhabu kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(2) Endapo adhabu haijaelezwa katika Kanuni hizi kwa kosa lolote la kinidhamu, Mamlaka husika itatoa adhabu ya kusimamishwa masomo kwa muda usiozidi mwaka mmoja au kumfukuza Chuo.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni hii, Mamlaka husika inaweza kutoa adhabu nyingine yoyote tofauti na adhabu zilizoainishwa katika Jedwali la Pili kulingana na mazingira na ukubwa wa kosa.

Makosa ya jinai

34.-(1) Kosa lolote la jinai chini ya sheria yoyote, lililofanywa na mwanafunzi, litachukuliwa kuwa kosa la kinidhamu chini ya Kanuni hizi na hatua za kinidhamu zitachukuliwa ipasavyo.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1),

Mshauri wa Wanafunzi au Afisa Ustawi wa Jamii anaweza, pamoja na hatua za kinidhamu zilizochukuliwa, kuripoti kosa la jinai kwa mamlaka husika kwa hatua zaidi za kisheria.

## SEHEMU YA TISA
## MASHARTI MENGINEYO

Matumizi ya sheria nyingine za Chuo

35.-(1) Kanuni hizi zitasomwa pamoja na Sheria na kanuni nyingine za chuo zilizopo.

Mwanafunzi kurejea Chuo baada ya kusimamishwa.

36. Mwanafunzi yeyote anayerudi kuendelea na masomo katika Chuo baada ya kusimamishwa chini ya Kanuni hizi, atawajibika na athari zote zitokanazo na kusimamishwa kwake.

Usalama maeneo ya Chuo

37.-(1) Mwanafunzi ataonesha kitambulisho katika maeneo yote wakati wote atakapotakiwa kufanya hivyo na afisa aliyeidhinishwa.

(2) Mwanafunzi atatakiwa kuonesha na kuvaa kitambulisho chake wakati wote akiwa katika maeneo ya Chuo.

(3) Lango kuu la Chuo au njia nyingine za kuingia Chuo zitafungwa saa 6:00 usiku hadi saa 11:30 alfajiri.

(4) Chuo hakitawajibika na uangalizi na usalama wa mali yoyote ya mwanafunzi.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 23(2))*

FOMU YA KUKIRI KOSA

Mimi (*Jina la mwanafunzi mtuhumiwa*), mwenye Namba ya Usajili …………………ninaelewa kuwa kukiri kwangu hakukusababishwa na ushawishi, tishio wala ahadi ya aina yoyote ile. Kuwa, kukiri kwangu ni kwa hiari, na kuwa kunaweza kutumika kama ushahidi dhidi yangu mbele ya Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi au Kamati ya Rufaa ya Nidhamu kwa Wanafunzi au mbele ya Mahakama. Kwa kuongezea, nimefahamishwa kuhusu haki zangu zote kwa mujibu wa Kanuni za Nidhamu za Wanafunzi za mwaka 2024.

*Maelezo ya kukiri kosa* ……………………………………………………….................

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………

……………………………………. ……………………..

Saini ya mwanafunzi mtuhumiwa tarehe ya kukiri kosa

*Tangazo la Serikali Na. 365 (Linaendelea)*

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 33(1))*

ADHABU KWA MAKOSA YA KINIDHAMU

| KANUNI | KOSA LA KINIDHAMU | ADHABU |
|---|---|---|
| 4 (a) | Mwenendo ambao unafanya au una uwezekano wa kusababisha uharibifu au vurugu kwa mtu au mali yoyote ndani ya Chuo ikizingatiwa kuwa, kitendo hicho kimefanywa na mwanafunzi dhidi ya mwanafunzi mwingine au afisa Chuoni au eneo lolote lililokodishwa au linalotambuliwa rasmi na Chuo. | Mwanafunzi atapewa onyo kali au kusimamishwa masomo kwa muda usiozidi mwaka mmoja na ataagizwa kulipa fidia kwa thamani ya mali iliyoharibika. |
| 4 (b) | Kutumia nguvu au vurugu au vitisho dhidi ya au kumshambulia mwanafunzi mwenzake au afisa wa Chuo au mtu yeyote ndani ya Chuo au eneo lolote lililokodishwa au linalotambuliwa rasmi na Chuo. | Mwanafunzi atasimamishwa masomo kwa muda usiopungua mwaka mmoja au kufukuzwa. |
| 4 (c) | Kitendo au mwenendo ambao unaweza kuzuia au kuvuruga uendeshaji wa shughuli ya kitaaluma, kiutawala au uchaguzi | Mwanafunzi atasimamishwa masomo kwa muda usiozidi mwaka mmoja wa masomo. |
| 4 (d) | Kuharibu, kuvuruga au kuteketeza mali ya Chuo | Mwanafunzi atasimamishwa masomo kwa mwaka mmoja, na ataagizwa kulipa fidia kwa thamani ya mali iliyoharibika. |
| 4 (e) | Matumizi yasioidhinishwa ya, au kuingilia, mfumo wowote wa kiteknolojia, umeme au huduma zingine za Chuo. | Mwanafunzi atasimamishwa masomo kwa muda usiozidi miezi sita, na ataagizwa kulipa fidia kwa thamani ya mali iliyoharibika au kuingilia huduma. |
| 4 (f) | Kumiliki mali ya Chuo bila ruhusa | Kutoa onyo kali na kumwagiza mwanafunzi kurudisha mali hiyo ikiwa na hali nzuri. Iwapo mali iliyorudishwa haitakuwa na hali nzuri, mwanafunzi atatakiwa kutoa fidia kwa mali aliyoharibu. |
| 4(g) | Kukataa au kushindwa kutii amri halali au maelekezo yaliyotolewa na afisa yeyote wa Chuo au amri kutoka kwa chombo chochote husika cha Chuo. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha mwanafunzi masomo kwa muda usiozidi miezi sita. |
| 4 (h) | Kutoa taarifa ya uongo kwa kujua. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi mitatu. |
| 4(1) (i) | Kushindwa au kukataa kuhudhuria kikao | Kutoa onyo kali au |

*Tangazo la Serikali Na. 365 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| | kilichoitishwa na chombo chochote chenye mamlaka kwa njia ya mdomo au maandishi. | kumsimamisha mwanafunzi masomo kwa muda usiozidi miezi sita. |
| 4 (j) | Kuzuia au kuingilia kwa makusudi kazi au mashauri yanayoendeshwa na afisa yeyote mwenye mamlaka au chombo chochote chenye mamlaka cha Chuo. | Kumsimamisha masomo mwanfunzi kwa mwaka mmoja. |
| 4 (k) | Kukataa au kushindwa kutoa ushahidi mbele ya Kamati ya Nidhamu kwa Wanafunzi au chombo kingine chochote chenye mamlaka | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi mitatu. |
| 4 (l) | Kukataa au kushindwa kuheshimu na kutekeleza hukumu, uamuzi au adhabu halali iliyotolewa na afisa yeyote au chombo kingine chochote chenye mamlaka. | Kumsimamisha mwanafunzi masomo kwa muda usiozidi mwaka mmoja au kumfukuza mwanafunzi. |
| 4 (m) | Matumizi ya lugha ya kashfa, matusi, chafu au ya kitisho baina ya wanafunzi au afisa au mwanajumuiya yeyote wa Chuo. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi sita. |
| 4(1) (n) | Kutenda kwa namna ambayo inaweza kushawishi au kuchochea vurugu miongoni mwa wanafunzi, iwe ndani ya Chuo au eneo lolote lililokodishwa au linalotambuliwa rasmi na Chuo. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi sita. |
| 4 (o) | Kufanya kitendo chochote kitakachosababisha au kinachoweza kumsababishia madhara ya kimwili au kisaikolojia mwanafunzi mwingine, au afisa au mwanajumuiya yeyote wa Chuo. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi mwaka mmoja. |
| 4 (p) | Kupiga kelele au kusumbua au kuwahamasisha wanafunzi au watu wengine kupiga kelele au kufanya usumbufu wa aina yoyote kwenye majengo ya Chuo au majengo yoyote yaliyokodiwa. | Kutoa onyo kali au kusimamisha masomo kwa muda usiopungua miezi mitatu. |
| 4 (q) | Kuunda au kuanzisha kikundi cha wanafunzi kisichoruhusiwa ambacho kinaweza kusababisha kuvunja umoja au kuleta vurugu. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi sita. |
| 4 (r) | Kuandaa, kushiriki au kuitisha kwa makusudi mkutano au kikao kinyume na sheria. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi sita. |
| 4 (s) | Kuchochea na kushiriki katika ghasia, mgomo, kususia madarasa au vurugu zozote au uchochezi wowote. | Kumsimamisha mwanafunzi masomo kwa muda usiozidi mwaka mmoja |
| 4 (t) | Kushawishi wanafunzi kugomea jambo lolote. | Onyo kali au kusimamisha masomo mwanafunzi kwa kuda usiopungua miezi sita. |

*Tangazo la Serikali Na. 365 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 4 (u) | Kuitisha au kufanya Baraza la Wanafunzi bila ruhusa. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha mwanafunzi masomo kwa muda usiopungua miezi sita. |
| 4 (v) | Kupanga na kushiriki kwenye maandamano yasiyo halali. | Kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi mwaka mmoja |
| 4 (w) | Kumwalika kiongozi wa serikali au wa kisiasa, mgeni rasmi, mshereheshaji, au mtu yeyote kutoka nje ya Chuo bila kupata ruhusa kutoka kwa Mshauri wa Wanafunzi au afisa mwingine yeyote mwenye mamlaka. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiopungua miezi mitatu. |
| 4 (x) | Kusambaza kwa maandishi au mdomo matamko ya kashfa kwa watu wengine. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiopungua miezi mitatu. |
| 4(y) | Uzembe au ubadhilifu wa fedha za Serikali ya Wanafunzi au chama, klabu, au kikundi chochote cha wanafunzi kinachotambulika. | Kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa mwaka mmoja na atatakiwa kurejesha fedha zilizofanyiwa ubadhirifu. |
| 4 (z) | Kiongozi wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara kuingia mkataba na mtu yeyote kinyume na Katiba ya Serikali ya Wanafunzi. | Kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi sita na binafsi atawajibika kwa deni au madai yatakayolimbikizwa chini ya huo mkataba. |
| 4 (aa) | Kukusanya fedha kwa ulaghai au kupokea fedha kwa udanganyifu kutoka kwa wanafunzi wenzake au mtu mwingine yeyote. | Kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa mwaka mmoja na atatakiwa kurejesha fedha alizokusanya kwa ulaghai au udanganyifu. |
| 4 (bb) | Kushindwa kulipa fidia kwa uharibifu au upotevu wa mali ya Chuo. | Kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiopungua miezi mitatu na atatakiwa kulipa fidia. |
| 4 (cc) | Kubeba silaha bila ruhusa au kibali ndani ya majengo ya Chuo au eneo lolote lililokodishwa au linalotambuliwa rasmi na Chuo. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiopungua miezi mitatu. |
| 4(dd) | Wizi unaofanyika katika majengo ya Chuo au eneo lolote lililokodishwa au linalotambuliwa rasmi na Chuo. | Kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiopungua miezi sita na mwanafunzi atatakiwa kurudisha au kulipa thamani ya mali hiyo. |
| 4 (ee) | Kughushi waraka au kusambaza waraka wa uongo au kuwasilisha waraka wa kughushi. | Kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiopungua miezi sita. |

*Tangazo la Serikali Na. 365 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 4 (ff) | Kosa ambalo linavunja Sheria ya Serikali Mtandao. | Kumfukuza mwanafunzi. |
| 4 (gg) | Kutumia dawa zozote haramu au sumu ya aina yoyote kwa mwanafunzi mwenyewe au mwanafunzi mwenzake au mtu mwingine yeyote. | Kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiopungua miezi sita au kumfukuza. |
| 4 (hh) | Kosa ambalo linavunja Sheria ya Makosa ya Kimtandao, | Kumfukuza mwanafunzi. |
| 4 (ii) | Kitendo chochote kinachofanywa na mwanafunzi ndani au nje ya Chuo na kupelekea kuharibu taswira ya Chuo. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiopungua miezi mitatu. |
| 4 (jj) | Kuendesha mkutano au kampeni ya uchaguzi nje ya muda uliopangwa. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi sita. |
| 4 (kk)(i) hadi (x) | Unyanyasaji wa kingono. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiopungua miezi sita. |
| 4(ll) | Kutoa au kupokea rushwa ya Ngono | Kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda wa mwaka mmoja au kumfukuza. |
| 4 (mm) | Kujifanya mtu mwingine | Kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiopungua mwaka mmoja au kumfukuza. |
| 4(nn) | Kitendo chochote kinachofanywa na mwanafunzi akikusudia kuonesha ushiriki au utii wake kwa chama cha siasa. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi sita. |
| 4 (oo) | Kushawishi au kuchochea wanafunzi kugomea mihadhara, mitihani ya vitendo au kazi yoyote ya kitaaluma. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi mwaka mmoja |
| 4 (pp) | Kushindwa kusoma taarifa au matangazo kwenye ubao wa matangazo, mfumo wa habari wa wanafunzi, au tovuti ya Chuo au namna nyingine itakayotumika, au kushindwa kufuata maelekezo husika. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi mitatu. |
| 4 (qq) | Kosa ambalo linavunja Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. | Kumfukuza masomo mwanafunzi. |
| 4(1) (rr) | Kosa ambalo linavunja Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. | Kumfukuza masomo mwanafunzi. |
| 4 (ss) | Kuingilia pasipo uhalali mchakato wa uchaguzi wa Serikali ya Wanafunzi. | Kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiopungua miezi sita. |

| | | |
|---|---|---|
| 4 (tt) | Kuunda au kuanzisha chama, klabu au kikundi cha wanafunzi bila ruhusa kutoka kwa Mshauri wa Wanafunzi, afisa Ustawi wa Jamii au chombo kingine chochote chenye mamlaka. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi mitatu. |
| 4 (uu) | Kushindwa kuonesha au kukabidhi kitambulisho cha uanafunzi inapotakiwa kufanya hivyo na afisa mwenye mamlaka. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi mitatu. |
| 4 (vv) | Kutokupitisha kwa Mshauri wa Wanafunzi au afisa Ustawi wa Jamii mawasiliano yoyote rasmi ya kwenda nje ya Chuo kwa mwanafunzi yeyote au kiongozi wa Serikali ya Wanafunzi ya Chuo cha Elimu ya Biashara. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi mitatu. |
| 4(ww) | Kushindwa kurejesha mkopo au deni baina ya wanafunzi au mtu mwingine yeyote. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi mitatu na kurejesha mkopo au deni. |

## ADHABU KWA MAKOSA YA KINIDHAMU YANAYOHUSIANA NA UVAAJI WA MAVAZI WA WANAFUNZI

| KANUNI | KOSA LA NIDHAMU | ADHABU |
|---|---|---|
| 5<br>(a) hadi (q) | Mwanafunzi yeyote atakayevunja Kanuni ya 5 (1) (a) hadi (q). | (a) Mwanafunzi atazuiwa kuingia kwenye majengo ya Chuo au majengo yoyote yaliyopangwa na Chuo;<br>(b) Mwanafunzi atazuiwa kuingia kwenye ofisi za Chuo, kumbi za mihadhara au madarasa, maktaba, maabara na mikusanyiko yote rasmi; au<br>(c) Mwanafunzi atasimamishwa masomo kwa muda usiozidi miezi mitatu. |

## ADHABU KWA MAKOSA YA KINIDHAMU YANAYOHUSIANA NA MALAZI

| KANUNI | KOSA LA NIDHAMU | ADHABU |
|---|---|---|
| 6 (a) | Kupangisha chumba katika mabweni ya Chuo au malazi mengine yaliyokodiwa au kutambuliwa na Chuo kwa mtu mwingine | Kumwondoa mwanafunzi bwenini bila kumrudishia malipo ya pango. |
| 6 (b) | Kuishi kwenye bweni la Chuo au malazi mengine yaliyokodiwa au kutambuliwa na Chuo pasipo uhalali. | Kulipa 30% ya malipo ya mwaka ya pango na kufukuzwa bwenini au malazi husika |
| 6 (c) | Kutumia majengo ya mabweni kwa ajili ya matukio ya kijamii bila kupata kibali cha Mshauri wa Wanafunzi au afisa ustawi wa jamii. | Kumwondoa mwanafunzi bwenini bila kumrejeshea malipo ya pango. |

*Tangazo la Serikali Na. 365 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 6 (d) | Kuchangia chumba na mwanafunzi wa jinsi tofauti | Kumwondoa mwanafunzi bwenini bila kumrejeshea malipo ya pango. |
| 6 (e) | Kupika chakula bwenini pasipo kibali cha maandishi kutoka kwa Mshauri wa Wanafunzi au afisa ustawi wa jamii. | Kumwondoa mwanafunzi bwenini bila kumrejeshea malipo ya pango. |
| 6 (f) | Kuingilia au kuhamisha samani au vifaa vya aina yoyote kutoka bwenini bila ruhusa ya Mshauri wa Wanafunzi au afisa ustawi wa jamii. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi mitatu.na atatakiwa kulipa kwa uharibifu au upotevu wowote wa kifaa au samani hiyo. |
| 6 (g) | Kutumia baraza, dirisha au ukuta kwa ajili ya kuanika nguo au ufuaji wa aina yoyote. | Kutoa onyo kali. |
| 6 (h) | Kuingiza bwenini friji, mashine ya kukausha, friza au kifaa chochote cha kupikia pasipo kibali cha maandishi kutoka kwa Mshauri wa Wanafunzi au afisa ustawi wa jamii. | Kumfukuza mwanafunzi bwenini bila kumrudishia malipo ya pango. |

| | | |
|---|---|---|
| 6 (i) | Kuondoka bila kumkabidhi vifaa vya malazi kwa afisa mwenye mamlaka. | Kutoa onyo kali na kumwagiza mwanafunzi kukabidhi vifaa vya malazi. |
| 6 (j) | Kumzuia afisa wa Chuo au mtu yeyote aliyeidhinishwa kuingia chumbani kwa ajili ya ukarabati, ukaguzi au shughuli nyingine kama iliyoamuriwa. | Kumfukuza mwanafunzi bwenini bila kumrudishia malipo ya pango. |
| 6 (k) | Kutumia vifaa vya muziki na vyombo vingine vinavyotoa sauti bwenini na kusababisha usumbufu kwa wakazi wengine. | Kutoa onyo kali au kumfukuza mwanafunzi kwenye chumba bila kumrudishia malipo ya pango. |
| 6 (l) | Ulevi au uvutaji wa sigara kwenye bwenini | Kutoa onyo kali au kumfukuza mwanafunzi kutoka kwenye chumba bila kumrudishia malipo ya pango. |
| 6 (m) | Kuwakaribisha wageni wa jinsia tofauti bwenini baada ya saa nne usiku. | Kutoa onyo kali au kumfukuza mwanafunzi katika chumba bila kumrudishia malipo ya pango. |

ADHABU KWA MAKOSA YA KINIDHAMU YANAYOHUSIANA NA MGAHAWA NA JIKO

| KANUNI | KOSA LA NIDHAMU | ADHABU |
|---|---|---|
| 10(1) | Kuingia jikoni kwa mtoa huduma za mgahawa bila ruhusa ya mtoa huduma au Mshauri wa Wanafunzi au afisa ustawi wa jamii. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi mitatu. |

*Tangazo la Serikali Na. 365 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 10(2) | Kuchukua chombo au kitu chochote kutoka mgahawani au eneo lolote ndani au nje ya Chuo ya Chuo bila cha mtoa huduma, Mshauri wa Wanafunzi au afisa ustawi wa jamii. | Kutoa onyo kali au kumsimamisha masomo mwanafunzi kwa muda usiozidi miezi mitatu.na mwanafunzi atatakiwa kurudisha vyombo au vitu hivyo vikiwa na hali nzuri au kulipa fidia kwa uharibifu wowote. |

Dar es Salaam,
23 Aprili, 2024

WINEASTER S. ANDERSON
*Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi*